



Bahati aliishi katika nchi ya Sususu. Alikuwa binti wa mfalme. Wazazi wake walikuwa watawala wa Sususu.



Mvua haikunyesha kwa muda. Nchi ya Sususu ilikabiliwa na ukame kwa muda mrefu. Watu hawakuwa na chakula wala maji.

Mimea ilikauka. Wanyama walitaabika bila maji.



Taabu za wanasususu zilifika kwa mfalme.  
Mfalme na washauri waliwaza wafanye nini.  
Waliitisha kikao kujadili hali ile.




Bahati alipenda kukaa karibu na baba yake mfalme wa Sususu. Alihudhuria vikao alivyofanya mfalme na washauri wake.



Mfalme alipojadili tatizo la ukame na washauri wake, Bahati naye aliwaza afanye nini kutatua matatizo ya nchi ya Sususu.



Bahati alipata wazo. Alitaka kumwambia baba  
yake, lakini hakumpa nafasi kwa sababu  
Bahati alikuwa mdogo sana.



Bahati alikwenda kwa mama yake, ambaye  
alikuwa malkia wa Sususu.

Malkia alimsikiliza na kuahidi kumsaidia.




Malkia alikwenda kwa mfalme na washauri wake. Aliwasih i wasikilize wazo la Bahati.



Mfalme wa Sususu alimpa Bahati nafasi ya kuongea mbele ya washauri. Bahati alisimama mbele ya baraza lile na kueleza wazo lake.



Aliwaeleza watu wa Sususu  
wazuie maji ya mvua.  
Wasiyaache yote yaelekee  
mtoni. Kisha wachimbe  
bwawa la kuyahifadhi.



Pia, wazuie maji ya mto na kuyaelekeza bwawani. Maji ya bwawani yatawasaidia hasa kipindi cha ukame.

Mfalme na washauri walifurahishwa na wazo la Bahati. Walipanga kuwaeleza wananchi wa Sususu ili walitekeleze.



Bahati aliwaongoza vijana wa Sususu.  
Walichimba bwawa kubwa. Wengine  
walichimba mifereji kuelekea bwawani.



Mvua ziliponyesha, mifereji ilipeleka maji bwawani. Mto nao ultiririsha maji bwawani. Bwawa lilikuwa na maji ya kutosha.



Maji yalifika Sususu. Watu walipata maji.  
Mimea ilinyeshewa. Wanyama walipata majani  
na maji. Bahati, Mfalme, Malkia na watu wote  
wa Sususu walifurahi sana.



